# Ripoti ya Mwaka 2013



**ATD Dunia ya Nne Tanzania**

**ATD Dunia ya Nne**

Imesajiliwa kwa namba 003447 chini ya sheria ya Asasi zisizo za kiserikali ya mwaka 2002

S.L.P. 61786, Dar es Salaam – Tanzania

atd.tanzania@gmail.com

Tovuti ya Kiingereza: www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html
Tovuti ya Kiswahili: www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html

# Utangulizi wa maudhui

Utangulizi....3
Sehemu cha kwanza – ATD Dunia ya Nne - Tanzania....4
1. Pamoja katika Utu....4
2. Muundo wa ATD Tanzania....4
2.1.Wanaharakati....5
2.2.Rafiki....5
2.3.Timu....5
2.4.Kundi la washauri....5
2.5.Kundi la vijana rafiki....6
3. Taswira yetu, kuutokomeza umaskimi uliokithiri....6
4. Tunafanyaje kazi....7
4.1.Kusikiliza kwa makini na kuelewa....7
4.2.Kuwa pamoja na kutafakari pamoja....7
4.3. kutafuta ufumbuzi....7
5. Tunakanyia wapi kazi?....8
5.1.Tandale....8
5.2.Tegeta (Kunduchi and Boko)....8
5.3.Soko la Samaki, Magogoni....8
Sehemu ya pili- Kazi zetu kwa mwaka 2013....9
1. Vipaumbele na miradi ya ATD Tanzania....9
2. Maelezo ya miradi ya ATD na harakati katika mwaka 2013....10
2.1. Tathimini, Mipango na Malengo kwa wakati ujao....10
2.2. Upatikanaji wa Elimu ya msingi....11
2.3. Watoto kupata vyeti vya kuzaliwa....12
2.4. Watu wazima kujifunza kusoma na kuandika....12
2.5. Maktaba ya Mtaa....12
2.6. Siku ya Kutokomeza Umaskini Uliokithiri Duniani....13
2.7. Majarida....13
Sehemu ya tatu- Mwelekeo kwa mwaka 2014....14
Viambatanisho- taarifa ya mapato....15

# Utangulizi

Haya ni marejeo ya yanayokumbushia kazi na mafanikio ya ATD Dunia ya Nne Tanzania katika mwaka 2013.

Tulipata moyo kutokana na juhudi tulizoziona kwa wazazi wenye hali ya umaskini jinsi wanavyojitoa katika kutafuta haki zao kwa kuwatafutia watoto wao vyeti vya kuzaliwa na kuwapeleka shule. Tunaeneza ujumbe wa harakati zetu. Maono yetu, ni kuhusu umaskini uliokithiri Tanzania na nchi nyingine. Kwa pamoja watu wazima walijifunza kusoma na kuandika, na kuwasomea vitabu watoto na kufanya nao shughuli za ubunifu. Vijana kutiana moyo katika mafanikio ya masomo yao na kujitoa wenyewe kwenye jamii zao.



Hatuwezi kukataa kama watu maskini sana kwenye jamii zetu wanaendelea kukumbana na ugumu siku hadi siku, kutafuta sehemu salama kwa watoto wao. Kufahamu kama watakuwa na chakula leo, kuwa na furaha katika mafaniko yao. Dimbwi la umaskini uliokithiri linameza matumaini yote ya watu wanaoishi kwenye umaskini, sasa hatuwezi kushindwa katika changamoto zinazotukabili leo, kuhakikisha watu wote wanaishi katika amani na utu.

# Sehemu cha kwanza – ATD Dunia ya Nne - Tanzania

ATD Dunia ya Nne ni shirika la Kimataifa lisilohusiana na dini wala siasa, lilianzishwa huko Ufaransa mwaka 1957. Kwa sasa lina wanachama wa kudumu katika nchi 32 kwenye mabara matano. Watu wanaoishi kwenye umaskini uliokithiri ndio sehemu ya kati ya harakati zetu, kwa kushiriki katika kutatua na kuushinda umaskini uliokithiri, pamoja tunasimama kwa haki za wote, kuanzisha ufahamu/uelewa wa uma na kushawishi sera za uma. Likiwa shirika la Kimataifa kwa muda wa miaka 50, limefanikiwa kupata ujuzi mkubwa wa kujifunza mambo mengi kutoka nchi nyingi zenye utamaduni tofauti, ujuzi huu hujadiliwa kwa kutumia njia tofauti, kama vile mikutano, taarifa na mitandao.

## 1. Pamoja katika Utu



Maneno haya ATD- “Pamoja katika utu” yanaelezea kwa kifupi sisi ni nani tunataka nini na jinsi tunavyo fanya kazi zetu. “Pamoja” inaeleweka, kwani linatufahamisha kuhusu umoja wa shirika, pia ulazima wa kushirikiana katika juhudi za kila mmoja ili kufikia malengo.

Fikra ya “Utu” inachanganya sana, lakini muhimu ni kama moyo wa ATD. Wanaharakati na marafiki hueleza kwamba “Utu” hupelekea kila mwanaadamu kuwa na thamani, pia kila mmoja anastahili kuheshimika. Utu ni asili ya binaadam, kwani kila mtu ana utu. Vile vile, katika hali fulani, binadamu hawaheshimiani.

## 2. Muundo wa ATD Tanzania

Shirika lilianza kufanya kazi hapa nchini mwaka 1999 na lilisajiliwa kama Shirika lisilo la kiserikali mwaka 2009. Chini ya Sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya mwaka 2002. Namba yake ya usajili NGO/00003447. Ni sehemu ya Shirika la Kimataifa la ATD Dunia ya Nne.

ATD Tanzania siyo Shirika la utawala. Lina wanachama wa tabaka zote na vikundi vyenye majukumu mbali mbali vyenye mshikamano thabiti.

## 2.1. Wanaharakati



Wanaharakati wanaishi katika umaskini uliokithiri. Wanao ujuzi wa kupambana na umaskini katika maisha yao ya kila siku pia wakiwasaidia wengine kuushinda umaskini. Wanajihusisha na miradi. Wengi wanaishi Dar es Salaam lakini wengine wapo mikoani.

## 2.2. Rafiki

Rafiki ni watu ambao siyo lazima wawe wamekumbana na hali ya umaskini bali wamejenga uhusiano baina ya jumuia au kazi zao na watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri. Wengine wako kwenye vikundi vingine. Wanayo shauku ya kulisaidia shirika na kujitolea kushirikiana na watu maskini.

## 2.3. Timu

Timu husaidia wanaharakati na marafiki katika matukio na miradi mbalimbali. Pia ndio wasimamizi wa shirika, na pia huendeleza mawasiliano ya karibu na harakati za ATD kimataifa.

Mwaka 2013 ATD Tanzania ilikuwa na wanaharakati 6 wa kudumu: Watanzania watatu na watatu kutoka nchi za nje. Watatu wapo kwenye kikosi cha wanaharakati wa kudumu wa kujitolea. Waliobaki walikuwa wanafunzi. Kundi hili linawasaidia wanaharakati na rafiki katika shughuli na miradi mbali mbali. Timu hii inahusika kuendesha na kusimamia shughuli za ofisini na kuwa na mawasiliano ya karibu na Makao Makuu ya ATD huko Ufaransa.

## 2.4. Kundi la washauri



Kundi dogo la rafiki na wanaharakati wamekuwa wakikutana mara kwa mara kuanzia mwezi Septemba mwaka 2008. Wanachama hawa ni mashahidi na washauri kuhusu maendeleo ya Shirika hapa nchini.

Katika mikutano 9 iliyofanywa kwa mwaka 2013, kundi la washauri lilipokea na kujadili taarifa zinazoihusu ATD taifa na harakati za kimataifa. Kundi lilichangia katika kutathimini na kupanga mikakati.

### 2.5. Kundi la vijana rafiki

Tangu Januari 2010, kundi la rafiki vijana wa ATD hukutana na kutafakari kwa pamoja kuhusu kazi ya kijana katika kujenga dunia yenye haki sawa. Wanatoka katika mataabaka tofauti tofauti na wengine wanaishi nje kidogo ya Dar es Salaam.



Katika mwaka 2013, kundi la vijana marafiki walikutana kila mwezi. Walijadili na kusaidiana katika njia tofauti na kushiriki katika shughuli zilizofanyika katika maeneo tofauti. Mwezi wa kumi na mbili walianza kufanya maktaba ya mtaa kila jumamosi ya kwanza ya mwezi katika maeneo ya Tandale.

## 3. Taswira yetu, kuutokomeza umaskini uliokithiri

Lengo kuu la Shirika la ATD ni kuushinda umaskini uliokithiri ili kujenga jamii sawa yenye kuthamini utu na haki za binadamu. ATD inalenga kumsaidia maskini na familia maskini kwa kuwepo kwake kuanzia ngazi za chini na kuhusisha jumuia zilizo maskini na kuziwezesha kuutambua umaskini uliokithiri na kuweka taratibu za kukabiliana nao.

Inaeleweka kwa ujumla kuwa umaskini uliokithiri ni kukosa mtaji. Hii ni kweli kwani fedha inawezesha kupata vitu vya msingi na huduma kama vile chakula, maji, makazi au usafiri. Umaskini uliokithiri una wigo mpana. Hauwezi kupunguzwa kwa muelekeo wake wa kiuchumi.

Wanaharakati na marafiki huelezea kuwa umaskini uliokithiri ni hali ambayo inakufanya kuwa tegemezi, unatengwa na jamii, ambapo haki za binadamu haziheshimiwi, ambapo huwezi kuelezea mbele za watu na pia hakuna tumaini la kuwa na hali nzuri hapo baadaye.

# 4. Tunafanyaje kazi

Shirika la ATD linawasaidia watu wanaoishi katika umaskini ulio kithiri kupata haki zao na kujenga  uhusiano na watu na taasisi tofauti: Watu wanaoishi katika umaskini ulio kithiri ndio kiini cha shirika. Ndiyo maana wanashiriki katika muafaka wa kuushinda umaskini ulio kithiri.

## 4.1. Kusikiliza kwa makini na kuelewa

Wanachama wa ATD binafsi husikiliza watu wanaoishi katika umaskini ulio kithiri. Jambo hili ni muhimu kwani mara nyingi vilio vyao havisikiki, hata kama ni wao wanaoelewa ugumu wa hali yao. Hii ni sehemu ya utu; watu wote wana kitu cha kusema na wanayo haki ya kusikilizwa.

## 4.2. Kuwa pamoja na kutafakari pamoja

ATD inawaleta pamoja maskini na wasiokuwa maskini ili kukutana na kufahamiana , kutafakari kuhusu hali zao, kuchangia ushuhuda, kuelewa nini sababu na madhaara ya umaskini. Hii ni dhana ya kuwafanya watu kutambua wao sio pekee wanaoguswa na matatizo,umaskini sio asili, kwamba wanahaki, watu wengine wanaguswa na hali zao. Tunakutana pamoja ili kuwatia moyo na hali ya kujiamini.

## 4.3. Kutafuta ufumbuzi

Hakuna njia maalumu iliyo rahisi ya ufumbuzi wa jinsi ya kuushinda umaskini uliokithiri. Hii inatokana na kuwa na mifumo yenye dhuluma katika nyanja za siasa, jamii, uchumi na utamaduni. Kwahiyo kila hali iko tofauti na wakati mwingine ngumu. Lakini ufumbuzi upo. Kuwa pamoja kunawafanya kuwa imara. Hata hivyo wanatambua kuwa wanazo haki na kwamba wanaweza kuzipigania. Pamoja na kuelewa na kupata ushauri kutoka ATD wanalenga kufikia kupata ufumbuzi wa kudumu kuhusu maswala yao.



# 5. Tunafanya wapi kazi?

Hapa Tanzania ATD imejikita kufanya kazi katika maeneo matatu ya jiji la Dar es Salaam; huko Tandale, Tegeta (Kunduchi na Boko) na soko la samaki Magogoni. Kwa zaidi ya miaka 10 ATD imeanzisha uhusiano na watu wengi na familia zinazo ishi katika maeneo hayo.

## 5.1. Tandale



Nikitongoji cha Dar es Salaam kilicho kati kati ya Sinza na Manzese. Watu wanao ishi pale ni watu wa tabaka mbali mbali. Sehemu nyingine zina hali ya umaskini na zimechakaa. Kwa zaidi ya miaka 10 sasa , ATD imewezesha miradi tofauti na kuanzisha mahusiano na watu pamoja na familia 100.

## 5.2. Tegeta (Kunduchi na Boko)



Tegeta ni kitongoji kilichopo maili kama 20 kaskazini ya Dar es Salaam. Kipo karibu na maeneo ya machimbo ya kokoto kama vile Kunduchi na Boko mahali ambapo watu zaidi ya elfu moja wanafanya kazi ya kuvunja mawe au wanapakia kokoto kwenye magari. Watu wanaovunja mawe ni wanaume na wanawake, wazee na vijana na hata watoto. Wengi wao ni maskini sana. Ingawa wengi wanaamini kuwa ipo siku wataondoka, lakini hukaa pale kwa miaka mingi.

## 5.3. Soko la Samaki, Magogoni



Soko la Samaki Magogoni ni kubwa sana hapa Dar es Salaam. Zaidi a watu 300 hufana kazi hapa. Wanafanya kazi na biashara za kila aina kama vile kuuza mboga, vyakula, mkaa na kuni, barafu kupaa na kukaanga samaki n.k. Wengi wao ni maskini ambao kila siku wanatafuta shughuli ndogo ndogo ili wapate riziki. Kuna vyama 15 vinavyowakilisha makundi haya.

# Sehemu ya pili- Kazi zetu kwa mwaka 2013

## 1. Vipaumbele na miradi ya ATD Tanzania

Mwaka 2010 ATD ilipanga kuwa na vipaumbele vinne. Vipaumbele hivi vinaliwezesha Shirika kupanga shughuli zake na miradi. Ni vema kuelewa vizuri ATD inataka kufanikisha nini hapa Tanzania.

- **Kuwasaidia wanachama kuhusu maendeleo ya Shirika hapa Tanzania**

Maendeleo ya ATD na kuwawezesha wanachama (wanaharakati na marafiki) ni jambo muhimu kwani wanapaswa kuwa viongozi wa shughuli hapa Tanzania. Tutaona katika sehemu ya pili ya taarifa hii kuwa jambo hilo lilikuwa na mafanikio mwaka 2012.

- **Kupitia shughuli na miradi yetu, tunawasaidia watu maskini kupambana na changamoto wanazo kabilina nazo.**

Wanachama wa ATD wanachukua hatua madhubuti kuwasaidia maskini. Mwaka 2012 kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, ATD ilitekeleza miradi inayolenga kufikia haki za msingi: elimu kwa watoto, vyeti vya kuzaliwa na elimu ya watu wazima. Katika sehemu ya pili tuitaelezea mafanikio.

- **Kuanzisha uhusiano wa karibu na kanda na dunia**

Likiwa ni Shirika la Kimataifa, ATD linamawasiliano ya karibu na timu kutoka nchi mbali mbali. Linawasaaidia wanaharakati na rafiki kufahamu haki kuhusu umaskini ulivyo katika nchi nyingine. Inawawezesha kutambua kuwa majukumu yao ni sehemu kubwa katika kupambana na umaskini ulio kithiri.

- **Kuimarisha hali yetu ya kifedha na masuala ya utawala**

ATD inawajibika vizuri katika kudhibiti mambo ya utawala na fedha. Lina maadili imara ya kujiendesha. Kuhakikisha kuwa fedha hazitumiwi vibaya kwa shughuli zisizokuwa za maana. Ni jambo muhimu kwa ATD kujiendesha na pia kutekeleza mradi. Taarifa ya fedha inaelezwa kwenye kiambatanisho.

# 2. Maelezo ya miradi ya ATD na harakati katika mwaka 2013

Wanachama wa ATD waliendeleza harakati kwa juhudi katika miaka iliyopita. Kufanya kazi kwa pamoja, familia zinazoishi kwenye umaskini uliokithiri zilipata nguvu na uwezo wa kufikia haki zao katika elimu, kujua kusoma na usajili wa vyeti vya kuzaliwa. Tuliendelea kuimarisha harakati za ATD Tanzania na kundi la washauri na kundi la vijana. Mwisho, tulichambua kupanga matarajio ya ATD kwa miaka inayokuja.

## 2.1. Tathimini, Mipango na Malengo kwa wakati ujao

Wanachama wa ATD walishiriki katika njia tofauti tofauti za huu mchakato. Baadhi walishiriki katika mahojiano ya mtu mmoja mmoja ambapo waliweza kutoa mawazo na hisia zao kuhusu miradi ya ATD. Baadhi waliweza kushiriki katika vikundi vya mikutano ambapo walipata nafasi ya kuonesha hisia zao juu ya tathimini ya kazi na kufikiri kwa kina kuhusu mwelekeo wa ATD hapa Tanzania. Baadhi walikuwa sehemu ya kamati ndogo ambayo ilifanya kazi maalumu ya kuanzisha malengo ya harakati.



Mwisho wa mchakato, wanachama wa ATD walikubali kufuatia malengo ya miaka minne ijayo.

- **Thamani ya binaadamu wote ni sawa- kipaumbele kwa maskini**

  Kipaumbele cha ATD Dunia ya Nne ni kwenda hatua kwa hatua, bega kwa bega, na watu maskini katika vitu vyote tunavyofanya. Ili kujenga uwaminifu, ushirikiano mzuri na kuifungua mioyo, akili zetu na kujuana vizuri na kuendelea kuwatafuta watu wengine wasiokuwepo. Tunapaswa kuheshimu na kuzingatia vikwazo wanavyokutana navyo kila siku na kuitia moyo jamii kujua juhudi na namna ya kujenga jamii nzuri.

- **Kujifunza katika maisha**

  Ni ile shauku ya kujifunza kutoka kwa watu wanaoishi katika hali ya umaskini katika rika zote haiwezi kupungua. Ukiangalia maisha magumu wanayo kumbana nayo. Kiundani uelewa wetu ni juu ya sura nzima ya elimu na kujifunza maisha,huanzia nyumbani katikaka jamii, shuleni na kwa ujumla kwenye maeneo yanayotoa elimu. Kipaumbele kitakua kutambua zile juhudi wanazozifanya watu wanaoishi katika umasikini na vikwazo wanavyo kumbana navyo katika kufanikisha suala la ujuzi. Lazima kuwasisitizia kujifunza kwa furaha na kuwatia moyo kwa kushiriki katika mafunzo yao na si kwa kufanya mashindano.

- **Vijana – ndio taifa la kesho**

Katika kipindi cha ujana ni kipindi ambacho kila mmoja anataka kuonekana kuwa ni mtanashati na kujionyesha mbele za watu, lakini hukabiliwa na majukumu mazito ya kusaidia familia zao. Tutaendelea kuwatia moyo vijana kutoka matabaka tofauti kujitambua na kutimiza ndoto zao. Kuhakikisha kuwa juhudi zao zinatambulika katika jamii zao kama kujenga amani na kujenga taifa lao.

- **Dunia ni ya wote**

Harakati zetu, mtazamo wetu, ni kwa dunia, kwa maskini na matajiri, kwa binaadamu wote kuishi kwa amani, umoja, utu na njia nzuri ya maisha. Tutawawezesha watu kufahamu na kuzifikia haki zao za msingi. Katika kueneza ujumbe tutashirikiana mitazamo, kwa kuanza na majirani, jamii yetu na walio mbali. Tutadumisha mshikamano na kuunda urafiki baina ya watu na makundi na kupeana ufahamu, mawazo na ujuzi tulionao kwa manufaa ya wote.

## 2.2. Upatikanaji wa Elimu ya msingi

Upatikanaji wa Elimu ni haki ya mwanadamu. Tunaamini ni moja ya njia bora katika kupigana na umaskini. Ni ufunguo unaotoa taaluma, ujuzi na ushindani kufahamu nyanja mbalimbali za kimaisha, kuwa na usawa na aina tofauti ya watu, kuwa na hali ya kujiamini, kuwa na uwezekano wa kupata ajira na kwa watoto kufahamu na kuhisi ni sehemu ya jamii.



Katika miaka iliyopita, ATD ilisaidia watoto walio maskini mno kupata elimu ya msingi na sekondari. Kwa mwaka 2013, tuliweza kusaidia zaidi ya watoto 50 kuanza kuhudhuria shule mara kwa mara. Kwa watoto wengi waliambatanisha vyeti vya kuzaliwa kusaidia katika hatua za usaili wa shule kwa miaka iliyofuata.

## 2.3. Watoto kupata vyeti vya kuzaliwa



Usajili wa vizazi ni muhimu sana kwasababu humfanya mtu “kutambulika kisheria” na kukutambua raia wa nchi. Na zaidi hupelekea watu kufikia na kupata kwa ukamilifu haki kama ya elimu au ajira iliyo rasmi. Wazazi walituambia ni muhimu kwa watoto wao kuwa na nyaraka hizi na wanaona ni hatua moja ya kuushinda umaskini uliokithiri.

Kwa mwaka 2013,tuliendelea na mradi wa vyeti vya kuzaliwa. Kwa Tegeta, wanaharakati wa ATD Venance, Shabani, Baba Meresiana walitoa msaada mkubwa kwa familia zilizo maskini mno kupata vyeti vya kuzaliwa. Kwa Tandale wazazi walihamasishana kuzishinda changamoto na kufuatilia karatasi muhimu kupitia nyumba tofauti. Kwa mwaka 2013, kwa pamoja tuliweza kusajili watoto 176.

## 2.4. Watu wazima kujifunza kusoma na kuandika



Si tu kutokujua kusoma na kuandika kuna hasara kubwa hasa katika maisha inakufanya kunyanyasika na kuwafanya watu kuoneakana hawana thamani katika haki zao. Ujinga hukufanya kushindwa kufanya vile vitu sahihi unavyo tazamia kama vile kusaini nyaraka, kusoma mabango ya matangazo muhimu na kujua basi lina kwenda wapi. Kwa kujua kusoma habari kama vile magazeti inaonyesha ni moja ya kutokomeza umaskini uliokithiri na kutengwa na jamii.

Tulikuwa na madarasa mawili ya watu wazima soko la samaki na Kunduchi. Kutoka soko la samaki Selemani na Hassan walikuwa ni viongozi wa darasa kati ya watu wazima 15 walishiriki katika kujifunza kusoma na kuandika. Kunduchi watu wazima 17 walishiriki katika darasa. Bi Agnes na Mr Kasian walifanya kazi kubwa katika kuwasaidia walio kuwa wakijifunza.

## 2.5. Maktaba ya Mtaa



Watoto wengi wanao shiriki kwenye Maktaba ya Mtaa wengi wao huwa hawana vitabu nyumbani vya kusoma hivyo maktaba ni sehemu yao maalumu ya kusikiliza hadithi kuchora na kuimba zaidi huwa fanya wafikirie hadithi wanazo soma na uhalisia wa maisha yao ya nyumbani wanayo kumbana nayo kwenye familia zao.

Maktaba ya Mtaa pia ni njia muhimu kwa ATD kuaminika kutambulika kwa jamia ya Tandale. Inatupa fursa sisi ya kukutana na wazazi wa watoto, kuwafahamu juu ya maisha yao, na juhudi wanazozifanya na changamoto wanazo kumbana nazo.

Katika mwaka 2013, kila Jumatano mchana huwa kuna kuwa na Maktaba ya Mtaa eneo la Tandale, kuna kuwa na wastani wa watoto 50 rika kuanzia umri wa miaka 3 kwenda 10.

## 2.6. Siku ya Kutokomeza Umaskini Uliokithiri Duniani

Kila mwaka duniani watu hukusanyika na kuadhimisha siku ya kutokomeza umaskini uliokithiri Tanzania iliadhimishwa kulingana na ujumbe usemao ''Tufanye kazi kwa pamoja ili kuwa na ulumwengu usio na ubaguzi''. Wanachama wa ATD walihojiwa na kutoa maoni yao namna ya kutokomeza ubaguzi ambayo yakawekwa wazi kwenye jarida siku ya kutokomeza umaskini.



Watu kutoka Tandale na wanaharakati walikutana na uongozi wa hospitali kuzungumzia juu ya kitendo alichofanyiwa mama mmoja hapo hospitali kilikuwa ni cha ubaguzi. Matokeo ya mkutano huo na utawala wa hospitali uliwakilishwa na wanachama wa ATD na kuwasomea shuhuda kwenye maadhimisho ya ATD 17 Octoba yaliyofanyika ofisini.

## 2.7. Majarida

ATD hutuma majarida kwa watu 480 hapa Tanzania. Walengwa ni watu wanaoishi katika umaskini ulio kithiri, watumishi wa serikali, viongozi wa dini na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali. Mara nyingi walio maskini sana hupelekewa kwa mkono na wanachama wa ATD huwasomea au hukutana na kusoma pamoja.

Lengo la majarida ni kuwaunganisha watu binafsi na taasisi zilizo na jukumu la kupambana na umaskini ulio kithiri, kubadilishana shuhuda na kueleweshana kuhusu haki ya maisha ili kufanya wale wanaoishi katika umaskini ulio kithiri wajione kuwa hawatengwi na kuruhusu sauti ya maskini isikike ili kuonyesha kuwa wao ndio wapambanaji wa kwanza katika mapambano dhidi ya umaskini uliokithiri.

# Sehemu ya tatu- Mwelekeo kwa mwaka 2014

Mwaka 2014 tutaendelea kufanya kazi katika vipaumbele vyetu vinne, kuzingatia yafuatayo:

## 1. Kipaumbele cha kwanza "kuwasaidia wanachama wa ATD katika maendeleo ya ATD Dunia ya Nne hapa Tanzania" tutafanya:

- Kuwahamasisha na kuwasaidia wanachama wa ATD kwa majukumu mbali mbali ya kujenga harakati hapa Tanzania.
- Kuwasaidia marafiki vijana wa ATD kujadili mambo yao na kuwakaribisha wengine kujiunga na kundi,
- Kuendelea kuboresha na kuongeza nguvu katika ushiriki wa wanachama wa kundi la washauri,
- Kuboresha mawasiliano na kulinda mawasiliano na marafiki wa ATD wanaoishi nje ya Dar es Salaam.

## 2. Kipaumbele cha pili "kusaidia, kupitia shughuli na miradi yetu, watu wasiothaminiwa katika changamoto wanazozipata" tutafanya yafuatayo:

- Kutunza mawasiliano na watu wanaofanya kazi katika ngazi za mamlaka, haswa wale wote wanaofanya kazi karibu na maskini watoa huduma kulingana na shughuli zetu,
- Kuwasaidia watu maskini kupambana na changamoto tofauti ili kupata haki zao za msingi,
- Kuendelea kuwasaidia watu maskini kuendesha shughuli kama vile kujifunza kusoma na kuandika, uandikishaji vyeti vya kuzaliwa n.k.

## 3. Kipaumbele cha tatu "kuunda uhusiano kikanda na dunia":

- Tutahakikisha kuwepo kwa kiswahili katika tovuti tofauti za harakati,
- Tutawakaribisha wawakilishi kutoka timu nyinge za ATD,
- Tutaendelea na mafunzo kuwaruhusu wanachama wa ATD Tanzania kuwakilisha na kujenga harakati ndani na nje ya nchi yao.

## 4. Kipaumbele cha nne "kuimarika kimapato na hali ya utawala":

-Tutaendelea kuchangisha fedha za kuendesha miradi yetu ndani ya Tanzania ili kukidhi mahitaji ya gharama zote.
- Kuendeleza uhusiano wetu mzuri na wafadhili ambao tumeujenga kwa muda mrefu na pia kutafuta njia nyingine za mapato kwa ajili ya miradi yetu.-
- Kuendelea na mlolongo wa kulinda nyaraka zote za kiwanja cha ATD Mwananyamala.
- Kufanya kazi na kuimarisha timu ya vijana wa Tanzania wanaojifunza ambao husaidia shughuli za timu. Pia watakuwa na nafasi ya kujitolea kwa ajili ya nchi yao na kufaidika kwa kujifunza.

# Viambatanisho - taarifa ya mapato

Miradi ya ATD ya usajili wa vyeti vya kuzaliwa na elimu ya watu wazima yalidhaminiwa na Better Lives, Hilfe fur Afrika, Diplomatic Spouses Group, Twiga Cement na Molly's Network. Tunapenda kuyashukuru haya mashirika kwa msaada wao. Tuna amini tutaendeleza ushirikiano katika siku zijazo.

Katika mwaka 2013, ATD ilifanyiwa tathimini na kupewa sifa kupitia Molly's Network. Kupitia tathimini walitambua juhudi za juu na ufanisi wa shirika. Dhumuni ni kutumia sifa hii kuendeleza mahusiano na washirika na wahisani, na kuwavutia washirika na wahisani wapya.

| | **Matumuzi** | **2012** | | | | **2013** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ***Euros*** | | ***Tz Shilings*** | | ***Euros*** | | ***Tz Shilings*** | |
| | ***1, Gharama za ofisi*** | | *8,565.44* | | *17,788,134* | | *7,665.36* | | *16,587,547* |
| 606110 | Maji | 48.80 | | 102,027 | | -16.86 | | -37,946 | |
| 606120 | Umeme | 138.38 | | 283,881 | | 260.36 | | 555,327 | |
| 606300 | Vifaa vidogo vidogo | 41.05 | | 85,976 | | 481.51 | | 1,029,869 | |
| 613200 | Kodi | 4,601.04 | | 9,533,757 | | 2,889.05 | | 6,227,578 | |
| | Kodi na uchakavu | 2,952.93 | | 6,174,634 | | 2,952.93 | | 6,452,887 | |
| 641110 | Mshahara wa mlinzi | 783.24 | | 1,607,859 | | 1,098.37 | | 2,359,832 | |
| | ***2, Huduma za kiofisi*** | | *3,051.30* | | *6,251,492* | | *1,893.09* | | *4,068,720* |
| 606320 | Gharama ndogo ndogo | 79.83 | | 154,986 | | - | | - | |
| 606400 | Vifaa vya ofisi | 740.91 | | 1,520,128 | | 523.06 | | 1,127,265 | |
| 615700 | Matengenezo mengine | - | | - | | 95.12 | | 204,395 | |
| 606800 | Ukaribisho | 675.36 | | 1,387,705 | | - | | - | |
| 618200 | Magazeti | 71.88 | | 148,696 | | 38.72 | | 82,513 | |
| 623700 | Uchapishagi / nakala | 419.79 | | 867,214 | | 756.31 | | 1,624,922 | |
| 626300 | Stempu | 362.80 | | 748,597 | | 292.68 | | 627,489 | |
| 626500 | Simu na mtandao | 269.68 | | 551,245 | | 187.59 | | 403,272 | |
| 616800 | Bima ya afiya | 120.95 | | 252,986 | | - | | - | |
| 637400 | Kulipa kodi nje ya nchi | 106.83 | | 218,543 | | -19.34 | | -42,546 | |
| 618500 | Vitabu | 203.27 | | 401,392 | | 18.95 | | 41,410 | |
| | ***3, Usafiri*** | | *6,001.30* | | *12,144,984* | | *3,110.13* | | *6,745,698* |
| 606150 | Mafuta/petroli | 385.61 | | 794,609 | | 240.16 | | 514,907 | |
| 615500 | Pikipiki matengenezo | 246.36 | | 510,295 | | 114.68 | | 246,331 | |
| 616700 | Kodi / bima ya pikipiki | 12.33 | | 24,979 | | 23.03 | | 49,994 | |
| 625110 | Usafiri nje ya nchi | 5,061.57 | | 10,209,808 | | 2,325.00 | | 5,062,480 | |
| 637200 | Viza na bima ya safari | 295.43 | | 605,293 | | 407.26 | | 871,986 | |
| | ***4, Shughuli*** | | *15,440.54* | | *31,043,112* | | *4,328.52* | | *9,333,004* |
| 613500 | Kodi | 85.95 | | 179,986 | | - | | - | |
| 650100 | Gharama za usafiri | 905.93 | | 1,888,513 | | 555.03 | | 1,196,816 | |
| 650200 | Fedha ya kujikimu kwa familia | 72.53 | | 149,445 | | 166.84 | | 363,481 | |
| 650250 | Mafunzo kwa vijana | 2,609.69 | | 5,375,117 | | 477.71 | | 1,039,181 | |
| 650300 | Chakula na vinywaji | 737.27 | | 1,537,870 | | 761.98 | | 1,643,195 | |
| 650400 | Matumizi kwa shughuli | 11,029.17 | | 21,912,181 | | 2,366.96 | | 5,090,331 | |
| | ***5, Timu, wanafunzi*** | | *26,246.35* | | *53,803,925* | | *14,059.30* | | *30,369,508* |
| | ***Mishahara (Watanzania wakujitolea)*** | | | | | | | | |
| 641100 | Mishahara ya watanzania wanaojitolea | 2,361.02 | | 4,835,875 | | - | | - | |
| 645320 | Michango ya wastaafu ndani ya nchi | 643.34 | | 1,314,641 | | 403.58 | | 863,072 | |
| 647810 | Mafunzo ya lugha | 676.50 | | 1,387,602 | | - | | - | |
| | ***Mishahara (Watanzania wanafunzi)*** | | | | | | | | |
| 641420 | Mishahara Watanzania wanafunzi | 2,569.00 | | 5,267,632 | | 2,330.09 | | 5,023,115 | |
| | ***Mishahara (Wageni wakujitolea)*** | | | | | | | | |
| 641400 | Mishahara wakujilotea nje ya nchi | 12,387.00 | | 25,086,500 | | 5,323.01 | | 11,366,104 | |
| 645300 | Michango wakujilotea nje ya nchi | 7,602.36 | | 15,896,681 | | 6,002.62 | | 13,117,217 | |
| 648100 | Matumizi ya ziada ya wajiliwa | 7.13 | | 14,994 | | - | | - | |
| | ***6, Gharama za benki*** | | *149.13* | | *304,638* | | *106.25* | | *228,663* |
| 627100 | Huduma za benki | 149.13 | | 304,638 | | 106.25 | | 228,663 | |
| | **Jumala ya Matumizi** | | **59,454.06** | | **121,336,285** | | **31,162.65** | | **67,333,140** |
| | Kubadilisha pesa za kigeni | 3,411.65 | | 7,017,911 | | 1,882.96 | | 4,096,210 | |
| | Kushuka kwa bei ya matengenzo ya ofisi | 509.52 | | 1,065,416 | | 1,101.10 | | 2,406,178 | |
| | Kushuka kwa bei ya pikipiki | 349.63 | | 731,083 | | 155.70 | | 340,242 | |
| | Mwisho kushuka kwa bei ya pikipiki iliyoibiwa | 286.89 | | 599,892 | | - | | - | |
| | Pesa ya msaada iliobaki | 1,480.36 | | 3,095,461 | | - | | - | |
| | **Jumula ya pesa tulioyekeza** | | **65,492.11** | | **133,846,048** | | **34,302.41** | | **74,175,770** |

ATD Dunia ya Nne

**Tanzania**

| | | 2012 | | 2013 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Mapato** | ***Euros*** | ***Tz Shillings*** | ***Euros*** | ***Tz Shillings*** |
| 708800 | Mauzo mengine / mchango | 26.47 | 54,998 | 468.27 | 989,981 |
| | Michango toka Ufransa | - | - | 160.00 | 349,639 |
| 754300 | Misada na michango ndani ya nchi | 1,406.53 | 2,889,952 | 135.77 | 287,925 |
| 744100 | Misada iliopokelewa nchini (DSG/BTC) | 13,477.63 | 27,230,400 | 5,829.10 | 12,499,967 |
| | Misada iliopokelewa nchini (SFD) | 15,000.00 | 31,365,292 | - | - |
| 755650 | Garama za michango | 2,353.93 | 4,853,855 | 1,478.11 | 3,171,063 |
| 754200 | Misada iliopokelewa Ulaya (Hilfe fur Afrika) | 1,000.00 | 1,941,456 | 1,000.00 | 2,156,255 |
| | Misada itakayotumika (DSG) | - | - | 1,480.36 | 3,234,954 |
| | Mabadiliko juu ya faida | 3,157.91 | 6,271,999 | 1,205.04 | 2,544,703 |
| | Misada toka ATD Dunia ya Nne - Terre et Homme de Demain | 29069.64 | 59,238,096 | 22545.76 | 48,941,283 |
| | **Jumula ya mapato** | **65,492.11** | **133,846,048** | **34,302.41** | **74,175,770** |

# Kwa taarifa zaidi

### Kitaifa na Kimataifa wasiliana nasi kwa:

**Makao Makuu ya Shirika Kimataifa**


**Paris : ATD Fourth World**
12, rue Pasteur
95480 Pierrelaye, France
tel : (33) 1 30 36 22 11 / fax : (33) 1 30 36 22 21


**Dar es Salaam, Tanzania**


**ATD Dunia ya Nne**
Mwananyamala A (Igusule street, n°34)
P.O. Box 61786 Dar es Salaam
E-mail : atd.tanzania@gmail.com


### Mitandao: Kimataifa,, 17 Oktoba, Tanzania…

**ATD Dunia ya Nne Harakati za Kimataifa -** mtandao wa kiingereza:

www.atd-fourthworld.org

**Siku ya Kuutokomeza Umaskini Uliokithiri Duniani** - mtandao wa kiingereza

www.overcomingpoverty.org

**ATD Dunia ya Nne** - ukurasa wa mitandao na nyaraka za marejeo...

kiingereza: www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html

kiswahili: www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html

**Joseph Wresinski, mwanilishi wa ATD Dunia ya Nne** -mitandao:

kiingereza: www.joseph-wresinski.org/Father-Joseph-Wresinski.html

kiswahili: www.joseph-wresinski.org/Unaye-mama-wewe.html